

(CKRC)



VERBATIM REPORT OF

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MOGOTIO
CONSTITUENCY ,HELD AT EMINING SECONDARY SCHOOL**

ON

5TH JULY 2002

CONSTITUTENCY PUBLIC HEARINGS, MOGOTIO CONSTITUENCY, HELD AT EMINING SECONDARY

SCHOOL ON 5TH JULY 2002

Present

Com. P.M. Wambua
Com. Zein Abubakar

Secretariat In Attendance

1. Fatuma Jama - Programme Officer
2. Wambeyi Makomere - Assistant Programme Officer
3. Lydiah Moraa - Verbatim Recorder

The meeting started at 10.25 a.m. with a prayer.

Prayer: (Speaker): (In Tugen)

Paul Kimoki: Asante sana kwa hayo maombi. Nikiwa mbele yenu nasimama kwa niaba ya Coordinator ambaye yuko upande wa Eldama Ravine kwa kazi kama hii na tunaanza saa hii hiyo tunaita public hearing ama kuchukua maoni yenu. Hivi saa hii bwana Commissioner tumekuwa tayari hapa na kabla sijawapea fursa, ninegenda pia kufanya introduction ya Committee wa the Constitutional Committee. Tuko nao wawili, mmoja wao ni hao wako mbele yenu na watasema majina yao.

Cheptieng: Mimi naitwa Cheptieng ambaye minatoka upande wa (inaudible) ndio nawakilisha kwa hiyo kamati ya kurekebisha katiba katika constituency.

Alfred Lagat: Mimi ni Alfred Lagat, ni mmoja wapo wa kamati na natoka upande wa Sirwa asante sana.

Paul Kimole: Nafikiri sijawambia jina langu pia jina langu ni Paul Kimok, nawakilisha Coordinator ambaye yuko nasi sasa hapo Eldama Ravine na pia ningekaribisha headmaster wa shule hii ili naye atukaribishe ama Chief kama yuko karibu. So mimi nampa programme Chairman ili ambaye ni host atuongoze.

Chairman: Wageni wetu wa siku ya leo, Commissioner hao wawili ambao wamefika siku ya leo, ninataka kusema ya kwamba munakaribishwa sana kataka tarafa hii ya Emining na vile vile katika uwakilishi wa Ubunge wa Mogotio. Sisi hapa tumekuwa tukitarajia nyinyi kwa muda mrefu, tumejitayarisha na kufuata taratibu ambao tulipewa. Wale ambao wanafundisha wamefundisha vile hawa watu ambao wako mbele yenu wanatakiwa kufanya na nafikiri yale ambayo wamepata ndio watasema wote wengi wao walikuwa wanasema muda ambao walipatiwa ulikuwa mfupi sana. Kama ungekuwa mrefu zaidi, wangukuwa na mambo ya kusema zaidi.

Najua ya kwamba wanajua vile wanataka kusema na pengine watasema kwa njia yao lakini wengi wao wameelewa ya kwamba sisi tunatakiwa kusema vile tunataka kukaa katika nchi hii ya Kenya. Kwa hivyo watafuata vile na mtasikia. Kwa hivyo hata nyinyi wale ambao mmefika siku ya leo ambao wanakuja kutoa maoni yao munakiribishwa vizuri na mukae na museme maneno yenu vizuri ili tuwe pamoja na watu wa Kenya wote. Kwa hivyo kwa hayo machache nasema ahsante sana na mimi narudisha microphone hii kwa Commissioners hili waendeshe kazi yao vile inatakikana. Asante sana.

Ahsante sana. Habari ya asubuhi?

Audience: Mzuri

Com. Zeuri: Jambo langu la kwanza la kufanya ni kukitambua kikao hiki kama kikao rasmi cha Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya kwa minajili ya kukusanya maoni ya Wakenya ili kurekebisha Katiba yetu. My first privilege is to declare this as an official function of the Constitution of Kenya Review Commission for the purpose of the collection of views of Kenyans in this constituency, Mogotio constituency, for the purpose of amending our Constitution. Hilo ni jambo langu la kwanza.

Ya pili ni kuwashukuru sana kwa kufika hapa na kuwaomba kwamba tuendelee na utulivu mulioonyesha ili tufanye kazi hii kwa nidhamu. Kama nilivyosema nimekitambua kikao hiki kuwa rasmi na tukisha kutambua kikao hiki kuwa rasmi kinakuwa na nidhamu fulani na nidhamu yake ni kwamba watu watakoruhusiwa kuzungumza ni wale wanaotoa maoni au ma commissioner wanaozungumza hapa. Ikiwa wewe una jambo lako lengine la kuzungumza, mnakwenda pale nje mnazungumza mnamaliza mnarudi ndani. Hilo ndilo jambo la kwanza na la pili ni kwamba kulikuwa kumeitwa headmaster ambaye ndiye mwenyeji wetu hapa na tunashukuru sana kwa kukubali kuwa mwenyeji wetu lakini alikuwa bado anashughulikia kutengeneza mambo pale nje lakini namuona amekuja. Kwa hivyo mimi sitaki tumrudie yeye baadaye nataka aje aseme mawili matatu tuu kwa sababu hatuna muda mrefu halafu ndiyo tuendelee haraka. Bwana headmaster.

Headmaster: Asante sana. Nimeshukuru sana ma -commissioners kuja hapa. Mimi ni host, nawakaribisheni hapa. Tulipopata barua yenye kwamba mnakuja tukafurahia sana sababu hili ni jambo la kihistoria. Kwa hivyo ningependa kuwaambia wenzangu ya kwamba hii nafasi tumepewa na serikali ya Kenya. Ile Constitution ya kwanza iliandikwa na watu wengine na hii ni yetu. Kwa hivyo tusiachwe nyuma, wale tunakuja tuseme yale tunayo moyoni ili wakati Constitution itaandikwa tutakuwa tumekuwa represented. Kwa hayo nawakaribisheni mjisikie nyumbani tafadhali tufanye yale tulikuwa tumekuja kufanya hapa ili tusiachwe nyuma na wakenya. Nimeshukuru sana.

Com. Zein: Ahsante sana bwana headmaster kwa ukarimu wako na kwa maneno yako mazuri, asante. Jambo langu la pili na la furaha, ningependa kumuomba Commissioner mwenzangu aliye na mimi ajitambulishwe aseme machache halafu mimi nitaendelea baada ya yeye kumaliza, asante.

Com: Wambua: Nitawasalimu kidogo kinyumbani *change thogol*. Ahsante sana. Mimi sitakuwa na mengi maanake yaliyotuleta hapa yanajulikana. Tumezuru sehemu hii kuchukua maoni ya wananchi na popote tulipofika tulipatiwa maoni ambayo yanafaa, hakukua na shaka. Tulipewa maoni na watu wakiwa wana furaha na walituambia yale ambayo wangelipenda yaingizwe kwa Katiba. Tulipoanza hii process tulisema itakuwa people driven kwa hivyo tungelipenda kila mmoja wenu ambaye amekuja hapa kutoa maoni atoe yale yote yako moyoni, atuambie jinsi angelipenda Katiba iandikwe kuhusu maswala fulani ambayo tayari Tume imewakilisha.

Kwa hivyo taratibu ambazo tutafuata hapa mtajulishwa na mwenzangu na tunatarajia kwamba tutakua na siku njema nanyi na tutatarajia kwamba yapo tumalize hiki kikao leo jioni ama wakati wowote ambao tutakapomaliza, nyinyi mtakuwa mumetueleza yale sehemu hii ya Emining mungelipenda yaingie kwa Katiba. Kwa hilo ni jambo la historia maanake haitaruhusiwa tena maybe hivi karibuni. Nafasi ni yako sasa usije ukasema sikupewa nafasi ya kutoa maoni yangu. Kwa hivyo muhakikishe ya kwamba muko huru na mtapewa nafasi ya kuzungumza yale ambayo mungependa yawekwe kwa Katiba. Kwa hivyo kwa kuwa sitaki kuchukua muda mtaelezwa utaratibu na mwenzangu. Sisi tuko na furaha kuwa hapa kuchukua maoni yenu na tunatarajia kwamba tutakopomaliza tutakua na furaha ile ambayo tulianza nayo Asante.

Com. Zein: Asante sana Commissioner Wambua, asante sana. Sasa mimi jambo langu la pili ni kuwajulisha kwenu maafisa au wafanyazi wa Tume tulioandamana nao na kazi gani wanafanya hapa. Ni muhimu nyinyi kufahamu ni kazi gani wanafanya hapa.

Nitaanza na kiongozi wao anaitwa Fatuma. Bi Fatuma pale yeye ni programme officer katika tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya na kazi yake kubwa ni kusimamia kazi yetu na kuona kwamba mambo yote yanayofanyika hapa yanaenda sawasawa. Lakini ya muhimu zaidi ambayo unafaa wewe kujua, yeye ana register na ana file. Unaona hiyo register anaonyesha? Hiyo register maanake kwamba ukishajiandisha pale ukaja ukaitwa kuzungumza ukimaliza kuzungumza ikiwa hakuna commissioner ana maswali kwako, utaondoka pale.

Ukiitwa unakuja unakaa pale unazungumza, ukimaliza kuzungumza ikiwa macommissioner hawana maswali unakwenda pale kwenye register una sign. Unaweza kuulizwa maswali kidogo pale kwenye register na ni muhimu maswali hayo uyajibu kwa sababu tunataka kujua ni wakenya wa aina gani, wa background gani wametoa maoni. Ni muhimu kwetu kujua, una-sign kwamba umetoa maoni. Ku-sign pale ni kwamba umeingia, umehudhuria kikao hiki. Ku-sign hapa maanake umetoa maoni yako na yamekua registered. Na ikiwa una maandishi utayawacha, yatawekwa kwa ile file. Kila constituency, kila hearing ina file yake kando.

Halafu yule Bwana Makomero yule yuko pale yeye kazi yake kubwa ni kufuatiliza mambo yanaoendelea hapa na kuyarekodi kwa mkono, ana rappotuer hii session nzima. Halafu Bi Moraa hapa kama unaweza kuwaonyesha hiyo tape recorder. ana

tape recorder, mbili ambazo zinafanya kazi. Kazi yeye ni kurekodi maneno yote yanayozungumzwa hapa. Sisi kule waswahili wa Mombasa tunasema hata ukikuna, ukifanya mmh pia unarekodiwa. Sababu kubwa ya kurekodi namna hiyo ni kwamba tunakuwa na recording mbili pamoja na zile za Ma-commissioner ni kwamba hatutaki kupoteza hata neno moja ambalo utasema wewe maanake ni muhimu katika ubadilishaji huu wa Katiba. Kwa hivyo usione pengine kuna wakati ambao Com. Wambua au mimi Com. Zein nimekaa hapa tumesita hatuandiki ukasema. “Mbona hawa hawaandiki mambo yangu muhimu?” Ni kwamba yanarekodiwa ni muhimu yanarekodiwa.

Kwa hivyo ni muhimu sana kama nilivyosema Bi. Moraa akiwa anarekodi ukija pale hata kama tumekuita kwa jina, ni muhimu utumie sauti yako mwenyewe utaje jina lako useme mimi ni fulani wa fulani ndio uanze kutoa maoni yako.

Jambo lingine la muhimu kufahamu ni kwamba ile register tunaandikisha pale ni orodha ya majina ya watu wote wanahudhuria kikao hiki. Kuna watu wa aina tofauti. Kuna wengine wanataka kuzungumza kutoa maoni na wengine hawataki. Ndio maana ukiulizwa pale wengine wameandikwa ni observer yaani wewe unataka kushuhudia tu na kusikiliza, kuwa shahidi nilikuwako siku ile ya kihistoria kama alivyosema headmaster Maneno haya yaliposemwa mimi nilikuwa shahidi nilishuhudia na kusikia. Kwa hivyo baadaye hata ukija kuangalia repoti utasema kweli haya yalisemwa au hayakusemwa. Wewe utakaa kwa nidhamu usikilize. Kuna wale wanaotaka kutoa maoni.

Kuna njia tatu za kutoa maoni na ni muhimu kufahamu hivyo. Njia ngapi? Tatu. Ya kwanza kabisa uwe na maandishi, you have a memorandum na ukiwa na maandishi yako ukiwa hutaki kusema lolote unaweza kwenda moja kwa moja kwa Bi. Fatma pale ukatoa maandishi yako, uka-sign register na ikawa umetoa maoni yako rasmi kwa Tume ya kurekebisha Katiba. Hiyo ni njia ya kwanza.

Njia ya pili, una yale maandishi yako lakini unataka kuzungumzia yaliyo muhimu katika maandishi yako kusudi watu wengine walio hudhuria hapa wafahamu unapendekeza nini kwa Tume ya kurekebisha Katiba. Na hiyo unaruhusiwa unakuja na memorandum yako hapa but we will not allow people to read. Na tuna sababu muhimu kusema hivyo. Kwa sababu yale maandishi ukitupa sisi tuna njia yetu ya kushughulikia yale maandishi rasmi Kwa hivyo tutayapitia tena kwa hiyo tunawaomba watu wasizungumze kuhusu yaliyomo yote pale. Uchague yaliyo muhimu, pointi kwa pointi u-highlight. You will just highlight the memorandum you will not read it to us. You just highlight, sijui kama tumefahimiana.

Njia ya tatu na ya mwisho ya kutoa maoni ni kwamba wewe huna maandishi unataka kusema kwa kauli yako kwa maneno yako yaliyo moyoni mwako na kichwani mwako. Unaruhusiwa kufanya hivyo lakini pia wewe unaezungumza namna hiyo tunataka useme mapendekezo, ni muhimu sana. Tunajua taabu na shida zilizoko nchini ni nyingi na tunatata uzitungumzie lakini si kwa kirefu. Utuambie mapendekezo yangu ni haya, kuhusu elimu mapendekezo kuhusu elimu ni haya. Lakini ukianza kuja kutuambia hapa hadithi ndefu; unajua siku hizi wazazi wana taabu nyingi kusomesha watoto wao. Nani asiyejua hivyo? Si sote tunajua hivyo. Kwa hivyo ili kuweka wakati uwe mzuri, tunataka mapendekezo, unasema kuhusu elimu mapendekezo yangu ni

haya. Na mapendekezo yako tutayachukua na kuyashughulikia kama mapendekezo mengine ya Wakenya wote bila kubagua na bila kupendelea.

Lingine la muhimu kufahamu ni kuhusu lugha. Lugha gani itaruhusiwa kutumika leo. Ya kwanza ni lugha yetu ya taifa, kiswahili, pia tunaruhusu watu kuzungumza kingereza na pia tunaruhusu watu kuzungumza lugha ya hapa. Watu wanazungumza nini hapa?

Tugen. Basi ikiwa watu wanazungumza Tugen, watu wanaruhusiwa hapa na kuna matayarishi ya mtu wa kutafsiri au sio hivyo? Nani atakuwa anatafsiri? Tuonyeshe kwa mkono. Huyu bwana atakuwa amekaa kiti cha hapa karibu na yule ikiwa kuna mtu anataka kutasfiriwa, anatasfiriwa.

Lingine la muhimu ni nini? Kwamba tunajua kutokana na mila, ada na desturi zetu sisi kama waafrika tukifika mahali kama hapa hatuzungumzi tu. Mtu ataanza, atasema 'napenda kuwashukuru sana Ma-commissioner kwa kufika hapa na tunataka pia kumtambua chief wetu, Bwana headmaster, Chairman wa Three C's' hiyo ndio mila na desturi lakini tunajenga Katiba na Katiba ni muhimu zaidi, mila na desturi leo tunaweka kando. Ukifika pale unasema mimi fulani wa fulani mapendekezo yangu ni haya, unaanza, unamaliza, unaenda. Sijui kama tunaielewana. Ukitaka kutuambia historia ya mzungu, alikuja vipi hapa, Tume ilikaa chini na kusoma historia hiyo. Jua ya kwamba tunajua sisi wengine lakini tukasema lazima tukae chini tusome hiyo historia. Kuhusu mashamba yalivyo-gawanywa, tunajua historia hiyo. Kwa hivyo ikiwa ni ardhi, ikiwa ni utawala, unatoa mapendekezo yako namna hiyo.

Kila mmoja wenu atapewa dakika tano. Utapewa dakika tano kwa sababu uzee wetu wa kazi umetuonyesha ya kwamba ukipewa dakika tano watu huchukua kama dakika nne, nne na sekunde kumi na tano na amemaliza. Zile zingine zote huwa ni hadithi sasa anaongezea. Na tunawahakikishia kwamba tuna uzoefu mzuri kwa sababu ukisha peana maoni, mikoa yote isipokuwa mikoa miwili, moja tunafanya sasa na wa mwisho tunakwenda Western. Kufikia hapa mimi huwa nauliza on behalf of this panel, kuna mtu yeyote mwenye swali? Ndugu yangu unaanza kuvunja nidhamu ya kikau kwa kuzungumza. Kuna mtu yeyote mwenye swali? Hakuna. Tungependa kumuita David.

Kitu kingine cha muhimu cha kusema ni kwamba hapa Mogotio kuna vikao viwili vinavyoendelea kwa hiyo usifikirie ni kikao cha hapa tu ukaona watu wengi hawajafika. Wanaweza kuwa wameenda kwenye kikao cha Mogotio town ambapo kuna panel ya Commission pia inaendelea. Bwana David Chetor.

David Chetor: The Commissioners, the team that accompanied the Commissioners and my colleagues who are at the center, I will start with the preamble. I am Mr. David Chetor, a primary school teacher in Emining division. I wish to present my personal Constitutional views to the Constitutional of Kenya Review Commission held here at Emining Secondary School. The views I am presenting are based on the questionnaire booklet sourced from the CKRC of March 2002. I am still on the preamble. The Constitution of Kenya should be able to bring together the Kenyan tribes, their shared values of freedom, equality, love, peace, unity and prosperity. The whole focus of diversity and development should be defined and protected by the Constitution. That is the preamble.

The constitutional supremacy – Democratic principles are predicated on the belief that everyone is potentially evil and needs to be held in check. Parliament therefore should be widely open and transparent to all Kenyans. Their debate should be covered by all media including TVs. The powers of checks and balances of the parliamentary process should not only be vested on the President but the Speaker as the monitoring figure and the Attorney General under judiciary to act as (inaudible). The Attorney General will be able to accuse a member of Parliament of wrong conduct during office before a competent tribunal. We do not want any other Parliament similar to the 8th Parliament which is associated with all societal evils like corruption, egocentrism, sleeping and non performance in Parliament, failure to attend sittings failure to perform in their constituencies.

Com. Zein: Pendekezo lako ni nini? You are talking about the history of 8th Parliament. What would you like to say?

David Chetor: As per the Parliament, I wish that the parliament should do its work. Then we come to citizenship. In citizenship, we have got these people from outside who have come to live in Kenya. If a person finds that he wants to live permanently in Kenya, then that person should have stayed and lived in Kenya for ten years and he has proved to be a worthy person to all Kenyans, to the Kenyan citizens. If that person misbehaves contrary to what the principles of registration are, then that person should be deported to his/her motherland country.

Political parties – in political parties, I find there is problem here. My personal view is that there should be two political parties in Kenya. The party that rules and the party that opposes so that that party which rules will have a strong opposition party.

About Legislature – I find there is also a problem here. We have MPs we have elected to represent us in Parliament but these MPs do not fully represent us. Why? Because when we have got sitting sessions we are told by the media that there was lack of quorum and whatever.

Com. Zein: Unatakaje?

David Chetor: Nitasema. So my suggestion is if an MP misses fifteen sitting sessions, fifteen sitting sessions in a month, that MP should have his salary cut and if such problems persist, then that MP should be recalled and perhaps the Speaker of the National Assembly declares the sit vacant and then by-elections are held.

The Executive – the person to hold this person should be a person of high integrity, must be well educated and widely versed with psychology. He must be a philanthropist like our current President, President Moi. He should be able to garner support during elections, 25% in at least five provinces.

Local government – the current two terms for mayors and council chairmen is enough. There is no problem on that one. The council should continue to operate under the central government, that is my suggestion. The councilor should be educated and

have good credentials of academic qualification because of what....

Interjection: (inaudible)

David Chetor: Okay, okay. I think because we are still having problems with illiteracy in Kenya, I propose I think the level that is proper is form four.

The electoral system and process – the Constitution should retain the simple majority as the basis of winning an election. A presidential aspirant should be declared President only and only if he has garnered 25% in at least five provinces in Kenya. I think as per the demarcation, Constitutional constituencies in Koibatek are okay.

Basic rights – Each and every person should have freedom of speech and association. Individual's life, property and rights should be protected. No one should endanger, risk or remove somebody's soul and if it so happens, he should face stiff consequences or death. Land and property rights – land should be owned by individual and because we have that scarcity of land, currently in Kenya I think we have got several kinds of acquisition of land. If the government is allocating land to people, let us say landless, if somebody has got 100 acres, that person should not be allocated any more land because already he has got 100 acres while we have got those ones with no land. Not even those people with 100 acres.

Cultural, ethnic and regional diversity and communal rights – we should have two national languages, Kiswahili and English. Cultural and ethnic values should be left to tribes for each belongs to them. Example, kikuyu cultural and ethnic values should not be termed as national values.

And then again, I have talked about management and use of natural resources – this one I think the executive should manage. Employees should be people of good credentials so that we have proper management of our natural resources.

Environment and natural resources – we have got this problem of pollution. Pollution of our environment. We have got this kind of dumping of waste material and I think this should be illegal and any person is found dumping and polluting the environment should be sued.

The rights of vulnerable persons or groups – we have got societal vices like rapists raping and doing other evil to the weaker sex. I think those people who are raping should be jailed for ten years and those ones who are not reforming should be castrated.

Com. Zein : Thank you very much Bwana Chetor, just hold on.

Com. Wambua: You suggested that there be two political parties in Kenya and you did not indicate to us whether these

political parties should be funded by the state because that is one of the questions which we asked. Can we have an indication as to whether you would want these political parties to be funded and whether they should be involved in any other activity other than mobilization for purposes of political activity?

David Chetor: I think as per the political parties funding, without corruption and other vices that get rid of monies from the public offers, the government is able to finance the political parties.

Com. Zein: - Thank you very much Bwana Chetor you took slightly longer than am willing to allocate others. I said five minutes, you took more than that but the reason why I allowed him to take more than that alipata bahati ya kuwa mtu wa kwanza, sio basi tafadhali register kwenye register yetu na utuachie memorandum tutaitumia hiyo. Wilson Kibet, karibu bwana.

Wilson Kibet: Mimi naitwa Wilson Kibet lakini sina memorandum ambao nimetayarisha lakini nitatoa maoni. Yaah, mimi kwa upande wangu sana ni mambo ya kubadilisha system ya serikali, yaani system yenye tunasimamia katika nchi hii ya Kenya. Kwa maoni yangu, sasa tuko kwa this presidential system. Now tunataka ibadilishwe ikuwe federal system.

Kwa upande mwingine wa pili ni upande wa mifugo. Tumeonelea mara nyingi tuko na shida kwa mifugo wetu. Tunataka iwekwe sheria kwa upande wa barabara, kuna magari yenye yanapita kwa barabara na mifugo. Mara kwa mara mifugo wanakanyagwa na mwenye gari anakuja kufuata mwenye mifugo tena anamfunga.

Com. Zein: Unapendekeza nini?

Wilson Kibet: Mimi napendekeza iwekwe sheria mwenye mifugo na mwenye gari, nataka iangaliwe mwenye atashika sheria atalipa. Kama ni mwenye gari atalipa mifugo wa mwenyewe alikanyaga.

Haya, ya tatu, mimi na- propose mambo ya land. Mimi, kwa upande wangu katika nchi ya Kenya, tunataka land kwa upande wa Rift Valley kama iko allocation of land free, ile inapewa wananchi wa Kenya ipewe wananchi wa Rift Valley. Nataka ipewe watu wa Rift Valley wenyewe, indigenous, sio wenye wanatoka province zengine. Kama ni ploti ama ni land, sawa basi.

Ya nne, mtu ana haki ya kununua shamba katika region yoyote within the Republic of Kenya lakini iko limitation, hawezi kununua more than ten acres. Haya, ya tano, nataka ku- propose mambo ya citizenship. Mtu akiwa si mwanakenya halisi kuzaliwa Kenya, awe amekaa nchi hii kweli kwa more than ten, fifteen years then awe mtu mwenye nidhamu na anaeleweka vizuri basi atapewa citizenship na aki-misbehave kuna haki ya kufukuzwa, kunyang'anywa hiyo citizenship.

Com. Zein: Muda wako umekwisha, umebakisha sekundi thelathini.

Wilson Kibet: Okay. Ya mwisho, mimi na-propose kwa upande wa administration. Mambo ya ma-chief, tunataka raia wa upande ya council of elders wawe wakiandika ma-chief na inategemea qualification yao, awe mtu amefikisha elimu ya form four.

So, ahsante.

Com. Zein: Asante sana Bwana Kibet, subiri kidogo kuna swali.

Com. Wambua: Wewe ulitaja kuhusu land, ulisema ya kwamba wale ambao wanatoka mkoa fulani ndio wawe wanapewa mashamba ma-allocation na ukataka Rift Valley peke yake. Je jambo hili lita-pply kila pahali ikiwa ni Eastern, ikiwa North Eastern iwe wale ambao wanatoka mkoa huo ndio wanapewa maanake ulisema Rift Valley peke yake? Pili, ukasema wale hawatoki mkoa huo wanaweza kupewa nafasi ya kununua mashamba na ma-plot lakini isipitishhe hekari kumi. Ningetaka kujua, ungesema nini kwa mashamba ambayo ni makubwa ambayo yanahusika na ukulima wa aina fulani kama commercial ranching, commercial farming? Nikipenda kununua shamba tuseme kama Laikipia for ranching nipewe tu heka kumi, nitafanyaje na hizo heka kumi maanake kazi ambayo naweza kufanya haiwezekani kwa hekari kumi?

Wilson Kibet: Okay, asante sana hilo swali kweli umeniuliza ni mzuri sana. Mahali mimi nimeonelea ya kwamba ililete shida ya land ni hapo umesema, umetaja mambo ya ranch. Hayo mashamba kubwa kubwa hatuwezi kukubaliana maana nimeona mashamba kubwa kubwa katika nchi hii yanasimamiwa na watu wachache na wanaweza kusema kweli anachukua shamba hii lakini wengi wa watu wako landless na haitawezekana mtu kuchukua elfu ishirini katika nchi hii na ikiwa watu wengine wa kutoka region hiyo hawana shamba hata acre moja.

Kwa hivyo mimi naonelea hapo haiwezi kua haki maana kila mtu anajiita mwanakenya na anajua kabisa katika region yenye, ako tuseme an example kama Central province kama mtu ako na twenty thousand acres na kuna mtu wa Central Province hana hata acre moja na anajiita ana shamba ya ranch. Hiyo haimaanishi nchi hii tulipata uhuru si wote. So tunataka tu-share national cake of this country – all Kenyans. Thank you.

Com. Zein: Lakini uliulizwa hiyo haki ya kupewa wenyeji mashamba iwe Rift valley peke yake au kama Coast, watu wenyeji pia wanapewa , Eastern wenyeji wanapewa?

Wilson Kibet: Ahsante. Mimi nasema siyo Rift Valley peke yake iwe Coast, iwe everywhere. Thank you.

Com. Zein: Sawa. Ahsante sana Bwana Kibet. Bwana Kibet anasema yeye akuandika lakini ametoa maoni yake vizuri, tunashukuru. Sasa namuita John Cheruiyot. Bwana John Cheruiyot karibu, una dakika tano kama wenzako utaje jina na uendelee tafadhali. Karibu.

John Cheruiyot: Our Consitutional Commissioners of Kenya ladies and gentlemen, infront of me is my presentation from

Sirwa Youth group and I will start with my proposals.

Parliament should have limited powers to control its procedures through standing orders. The Members of Parliament should not be a full time occupation so that they may be more effective. Age requirements for voting should be 18 years and above. For contesting parliamentary seat should be 21 years and should remain 35 years minimum for presidency. Both languages be tested and oral interviews on languages be requirement for parliamentary election. In addition, be a form four holder and above.

The Constitution should provide for moral and ethical qualification for parliamentary candidates. The people should have the right to recall their member of parliament if two thirds 67% of the voters pass a vote of no confidence. MPs should act on instructions from their constituents or parties. An independent Commission should determine the salaries and benefits of MPs. There should be special measures put in place to increase women participation in Parliament by having six of the twelve nominated members of Parliament for women.

Local government – Mayors and council chairmen be elected directly by the people. The current two year term of mayors and council chairmen to continue. The councillors to operate under the central government. The councilors to be given more powers to allow the council run smoothly without the chief officer having more say. The minimum education qualification for councilors be K.C.E., K.C.S.E. or form four and should pass language test requirements. There should be moral and ethical qualification for local authority seat, a letter for the same from the local elders to justify. The people should have right to recall their councilors if two thirds of the voters pass a vote of no confidence on their councilors. The central government should determine tape and words lost. The nominees should qualify for the post. The constitution to provide and guarantee security, health care, water, education, shelter, food and employment (inaudible) rights for Kenyans for a strong and healthy nation. The government should have the responsibility of ensuring that all Kenyans enjoy the basic rights such as education, security, health care, food shelter and employment. The specific issues which the Consitution should deal with are:

- 1) Health care: free medical services in dispensaries and health centers. There is need to have funds for complicated issues to assist pressing cases which require a lot of money which the common man cannot afford.
- 2) Education – free education from ECT centers to form four and that the government to employ ECT center teachers which will therefore lead to free and compulsory education and those who don't go to school to be disciplined.
- 3) Shelter – the government to provide shelter for the less fortunate so as to realize a mutual contribution towards nation building and reducing or eradicating poverty.
- 4) Food – the government to create national food security and subsidise farm inputs. The government to create other mechanisms such as irrigation projects and land reclamation to boost food production in this country.
- 5) Structure and system of government – there is need to adopt a parliamentary system of government in which a Prime Minister is appointed from the majority party in Parliament and President remains more or less ceremonial. In parliament

system, Parliament is the day to day source of government power. Apart from citizens and Constitution, no institution is above Parliament. The head of state is a symbol of national unity and considered to be a day to day politics but has a little real power. Thank you.

Com. Zein: Thank you very much John, just hold on.

Com. Wambua: Kidogo Bwana Cheruiyot, you say that the right to recall an elected councillor should be two thirds votes. We would want to know whether you have thought of the procedures of getting these two thirds votes. Is it a referendum, is it voting, is it collection of signatures? If you have not thought about it it is okay but if you have thought about it in the memorandum, please mention. Secondly, you did not talk about the right to recall the MP and the right to recall the President where he does not perform. You just concentrated on the councillors or these other elected leaders. Do you have any proposals in situations where the MP fails to perform, where the president does not perform as per expectations?

John Cheruiyot: I will start answering the question on the side of councillors because I have considered it so much. On the side of councilors, because the local authority should be the basic foundation of any government and for any good strong government in future we need to strengthen the foundation, that is why I would say sixty.

Com. Wambua: Sorry, I have understood but do you have proposals? If you have, just give them. If you don't have, it is okay.

John Cheruiyot: I don't have a written one.

Com. Wambua: Thank you very much.

Com. Zein: Asante. Please register. Eeh sasa namuita John Komen. Bwana John Komen, karibu.

John Komen : Asante sana kwa ma-commisioners na wananchi wenzangu ambao wamekuja kutoa maoni na kusikiza. Sina chochote ambacho kimeandikwa lakini nataka tuu kutoa maoni kidogo orally.

La kwanza ningetaka kutoa maoni kuhusu haki za watoto. Haki za watoto, inaonekana iko shida sana watoto na ambayo ni chokora ama street boys, wanatokana na wale watoto wanazaliwa nje ya ndoa. Watoto kama hao wanazaliwa na watoto wetu wa nyumbani ambao hawajaolewa na vile mimi nataka sheria ifanye kazi ni kwamba kwa kweli kila mtu anajua ya kwamba hakuna mtoto aliye na mzazi mmoja. Mtoto lazima awe na wazazi wote wawili. Kwa hivyo mimi ningetaka sheria itafute baba ya kila mtoto na awe responsible kwa maisha ya huyo mtoto. Kwa sababu kuna vijana wengine ambao wamekua bingwa, anazaa mtoto hapa na anazaa mtoto pale na wanawacha wakiumia. Kwa hivyo watafutwe ili pamoja na mama, iwe jukumu lao

kulea yule mtoto ambae amezaliwa.

La pili ni kuhusu umiliki wa mali. Katika Kenya hii kuna mahali ambapo mimi naona ubaguzi umefanywa na hasa kwa makabila mingi ndani ya Kenya, hawa wakalenjin ama wa Tugen wangu wakiwa mmoja wao. Mtu/mimi naweza, kwa mfano naweza kuoza nizae watoto wa kike kama wane, watano hivi. Ndugu yangu amefanikiwa kuwa na wanaume, kuchanganywa wanaume na wasichana na ndugu mwingine namna hiyo. Halafu baada ya mimi kuaga dunia au niende kwa bahati mbaya kulingana na kimila ambayo tumekua nayo, wasichana wangu wanatupwa nje ya shamba yangu na wavulana wa ndugu zangu wanakuja kuriithi mali. Hiyo, kabisa that is a crime.

Com. Zein: - Unapendekeza nini?

John Komen: Mimi napendekeza watoto wangu, wawe wasichana au wanaume wariithi mali yangu. Wawe na haki.

La tatu ni umilike wa ardhi. Katika Kenya kuna hii taabu ya kutokua na ardhi ama kua landless. Hii inatokana na sababu ya watu wengine wachache kuwa na shamba kubwa ambayo ingetoshoa wakenya wengi. Kwa hivyo pendekezo langu ni kwamba mtu awe na acre mia mbili ya ardhi ya juu kabisa na isizidi hiyo na ikizidi hiyo, ma-acre ambazo ziko juu iwe taxed by the government. One person awe na shamba moja peke yake acre mia mbili ya juu kabisa. Lngine ni mambo ya election date. Tarehe ya kufanya uchaguzi ifanywe kuwa sheria na iwekwe. Kama ni tarehe kumi kila December baada ya miaka tano, ikuwe namna hiyo ili mtu yeyote asicheze na hiyo na ikuwe namna hiyo. Kwa sababu kwa mfano kama wakati huu kuna msukosuko. Wananchi wanaambiwa siku ya kufanya uchaguzi utaongezwa na hii ni kitu ambacho kinapitishwa na watu wachache na watu waliowachagua wako bila kujulishwa, bila kujadiliana na hawa. Kwa hivyo ikuwe sheria ya kwamba tarehe ya uchaguzi (inaudible) iwekwe na isivunjwe.

Com. Zein: Umependekeza tarehe ya uchaguzi iwekwe ndani ya Katiba.

John Komen: Kwa Katiba ndiyo. Na kuhusu wabunge au ma-councillors ambao hawafanyi kazi yao vizuri wananchi wawe na right ya kuwaregesha nyumbani kwa kutokoa na imani na hawa na iwe ni collection of signatures, wapitishie kura ya kutokua na imani by 65% of the wananchi. Ahsante.

Com. Zein: Ni swali kidogo tuu mzee wangu. Tumesikia watu wengi wanapendekeza njia ya kuwarudisha ma MP au wabunge ambao hawatimizi wajibu wao kama wananchi wanavyotarajia na swali alilouliza mwenzangu kwa yule mwenzako aliyekuwa hapa, pengine niliulize kivingine. Unasema watu wakusanye sahihi za watu kiwango cha asili mia sitini na tano ya wapigaji kura wa eneo hilo, ziwe zinatoshwa kumrudisha nyumbani. Hivyo ndivyo unavyosema?

John Komen : Ndiyo.

Com. Zein: Je, kutakuwa kunatumika njia gani kuzuia njia kama hiyo isitumike vibaya?

John Komen: Huo uamuzi utoke tu kwa watu walio chagua huyo mtu na siasa ingine yeyote isiingizwe. Wenye kumchagua huyo mtu watoe maoni yao na wapitishie bila kuingiliwa na mtu mwingine yeyote kutoka nje.

Com. Zein: Kwa hivyo mtu anaweza akachaguliwa leo, yule alishidwa na yeye leo, (inaudible) kesho aende kuanza kukusanya sahihi?

John Komen: Maoni kama hayo yasisikizwe na mbunge apatiwe kwanza (inaudible) kama miaka miwili kama probation, asipotimiza hiyo aondolewe.

Com. Zein: Sawa mzee wangu. Sasa tunamuomba Bwana Jonathan Kimaru. Ningependa kutambua kuasili kwa mheshimiwa. Karibu bwana waziri.

Hon. William Morogo: Asante sana.

Jonathan Kimaru: Asante sana Ma-commissioners na wasikizaji wenzangu. Yangu ni maoni tu juu ya umaskini katika Kenya. Tunajua Kenya kuna umaskini mwingi. Yangu labda tu itakuwa upande moja

Com. Zein: Taja jina lako kwanza.

Jonathan Kimaru: Jonathan Kimaru. Ningependekeza ya kwamba wakulima wasaidiwe kwa sababu ukulima ni uti wa mgongo katika Kenya. Wapewe mkopo, wapatiwe soko kwa mimea yao ile inatoka shambani. Pili, waweze kujisimamia kwa sababu wakipata uwezo wa kujisimamia hawatasumbua serikali kwa kusema watafutiwe chakula, watafutiwe pesa ya school fees hata hii michango hatutakuwa nayo. Kwa hivyo hiyo ni pendekezo langu waangaliwe kabisa kwa sababu tusipoangaliwa tuko na shida.

Ingingine ni kwa mambo ya utawala na usalama wa nchi. Kuna hawa watu wanaitwa wazee wa mitaa. Hawa wazee wa mitaa wanafanya kazi nyingi sana hata ingawa ni wa kujitolea. Kwa hivyo ningeuuliza serikali iwaangalie kama watapewa kiinua mgongo, kidogo tu cha kuwezesha kuona kweli wako kwa kazi wanasaidia nchi. Kwa hivyo sina mengi, asante.

Com. Zein: Ahsante sana Bwana Kimaru.

Jonathan Kimaru: Ahsante sana.

Com. Zein: Tafadhali jiandikishe pale mzee wangu kama umetoa maoni kwa Tume ya kurekebisha Katiba. Bwana Kiplagat Chumo karibu mzee.

Kiplagat Chumba: *Kikureno Kiplagat Chumba.*

Translator : Mimi ni Kiplagat Chumba

Kiplagat Chumba: *Amache angalale Kalenjin.*

Translator: Anataka aseme kwa kilugha ya kalenjin.

Kiplagat Chumba: *Amoche angalal akobo imbarenik.*

Translator: Anataka kusema maoni kuhusu shamba.

Kiplagat Chumba: *Imbarenik cheikoitoi Serkali kokochinin biik chemotinyei.*

Translator: Anataka aseme mawazo yake kuhusu shamba ile serikali inataka kupatia landless.

Kiplagat Chumba; *Ngemoche kesomchilakok kokakikoito kobasang.*

Translator: Hizo mashamba Mzee anasema ya kwamba akitaka kuombea watoto na kadhalika, kufika pale anakuta kwamba hizo mashamba zimepeanwa.

Interjection: Zimepeanwa kwa nini? (inaudible)

Kiplagat Chumba: *Kikikoito eng olimbosang.)*

Translator: Imepeanwa nje.

Kiplagat Chumba: *Ngalekab imbar konyoljini kebchei eng gaa anan location.*

Translator: Kuhusu mashamba kama hayo, inatakikana kwamba iletwe nyumbani ama kwa location halafu kila mtu aone na atoe maoni yake kuhusu mashamba kama hayo.

Kiplagat Chumba: *Asikobit konyor akotkitikin chemotinyei.*

Translator: Halafu wale hawana mashamba wapate nafasi ya kupewa hata shamba kidogo.

Kiplagat Chumba: *Ngetiem kesom imbarenjuta kelechech makomitei.*

Translator: Siku hizi tukijaribu kuomba tunaambiwa hakuna mashamba.

Kiplagat Chumba: *Kikwongtosi kekas kele mito biik alake chekinyor imbarenik.*

Translator: Lakini tunashangaa unasikia kwamba kuna mwengine amepata shamba mahali fulani na kadhalika lakini hapa nyumbani tunaambiwa hakuna shamba. So tunashangaa watu kama hawa wanapitia njia gani ndio wapewe mashamba na siyo wale hawana mashamba.

Kiplagat Chumba: *Kakai konai councilaek akobo imbarenichuto asikomwoweche icheket.*

Translator: Tunataka councillors wawe na habari kuhusu mashamba kama hayo halafu councilors watuletee ripoti kama hiyo.

Kiplagat Chumba: *Motinye ngalekalak.*

Translator: Sasa sina mengi.

Kiplagat Chumba: *Kongoi neo .*

Com. Zein: Tafadhali mwambie Mzee kongoi sana, tumemshukuru sana, aende pale andikishe jina lake kwamba ametoa maoni kwa Tume ya Kurekebisha Katiba. Mheshimiwa waziri kama unaweza kutu-join hapa karibu ukae karibu hapa. Hapa ni mahali kwako karibu. Nafikiri unafahamu kwamba mheshimiwa (inaudible). Ningependa kumuomba bwana Job Cheruiyot afuatie.

Job Cheruiyot: Thank you very much the Commissioners, my name is Job Cheruiyot I have an oral presentation and mine will touch on the following: I will talk on provincial administration. I would like to make a proposal that the chiefs and assistant chiefs to seek nomination from the wananchi and actually beroted in (inaudible) together with the elders for interviews and he/she should have form four level of education and have moral and ethical qualification.

On education, I suggest that the government provides free education from pre-school to form four at least and specifically re-introduces the Kenya School equipment schemes to boost our education on special education needs for people with disabilities, they are assisted upto even tertiary institutions like colleges and public universities.

On management and the use of natural resources, the government should apportion benefits from the resources between the central government and the local community. In this case, the central government should take 70% so that it will boost in free education and the community to take 30%.

Environment and natural resources – the Constitution should also be amended to strengthen the protection of environment through the reforestation, and protection of water catchment areas. Thank you very much.

Com. Zein: Thank you very much bwana Job Cheruiyot, tafadhali uende pale u-sign register yetu kwamba umetoa maoni kwa Tume ye Kurekebisha Katiba. Sasa namwomba Isaiah Kimona Chemjor, karibu bwana.

Isaiah Kimona Chemjor: *Ngoliot netai go ngalekab timto.*

Translator: Neno la kwanza linahusu misitu

Isaiah Kimona Chemjor: *Ngotkomi timto nemoktoi kikoch biik chebo yoto.*

Translator: Kama kuna misitu mahali, wale watu wako karibu na hiyo misitu; hiyo misitu ni yao.

Isaiah Kimona Chemjor: *Ngoliot ake kobo bilotisiekab center.*

Translator: Lngine linahusu plots.

Isaiah Kimona Chemjor: *Makat kemetochi county council ngalekab bilotisiek.*

Translator: Wale watu lazima wahusike na plots ni county council.

Isaiah Kimona Chemjor: *Nyolunot korib county council asimoib biich alake eng oretab chorset kou biicho miNairobi ak alak.*

Translator: County council lazima wachunge maneno ya plots kwa sababu kuna zile ma-plots hazijajengwa so wale watu wakubwa wenye wako Nairobi wanaweza kuja karibu hapo waone kwamba kuna ploti hazijajengwa na wanyakue. Maneno kama haya hatutaki.

Isaiah Kimona Chemjor: *Ngaliotake kobo lakok cheimuch kesich komokororon keliek ak eunek.*

Translator: Lngine linahusu watoto. Mtoto anaweza zaliwa na hana mwili kamili, ni cripple. Serikali inaombwa isaidie wazazi wale wana mtoto kama huyo.

Isaiah Kimona Chemjor: *Kisomei serkali kotoret lakochoto engoretaketukul.*

